

Laweza kutengenezwa kwa mbaao na kupakwa rangi nyeusi ndani. Ukubwa wake waweza kuwa inchi 12 x 12 x 16 .

ZALISHA MARA KWA MARA


- Mara zote, peleka jike kwenye banda la dume
- Sungura anawezakuzaa nara nne hadi tano kwa mwaka
- Mimba huchukuwa siku 30—32
- Watoto watenganishwe baada ya siku 42

ULISHAJI WA SUNGURA

- Inapaswa kumlisha sungura wakati wote, usiku na mchana. Ufugaji mzuri unazingatia lishe bora yenye virutubisho muhimu
- Aina za vyakula Bora kwa sungura
- Malisho ya majani - marejea, mchicha, nk
- Malisho yanayotoa nguvu—pumba, nafaka, mchele ngano nk
- Malisho yanayotoa protin - mashudu, mikunde nk
- Vyakula mchanganyiko kwa ajili ya kuku vyafaa iwapo vitalishwa pamoja na najani

FURAHIA NYAMA BORA

Chinja sungura kwa ungalifu, Hakikisha damu yote imechurizika. Nyama ni laini, na yeweza kuokwa ku-kaangwa, kwa supu nk Namna ya kutengeneza ni chaguo la mlaji



FUGA SUNGURA, UPATE TIJA NA UFUHIE UTAMU WAKE.

Kimetayarishwa na Chuo Kikuu cha Sokoine Cha Kilimo.


*G.C. Kifaro
G.H. Laswai
I. I. Kerario
I. Kibasu
N. Madalla
B. Mayunga*

Kwa ushauri-zaidi onana au mwandikie Mkuu wa Idara

**Kitivo cha kilimo
Idara ya sayansi wanyama na uzalishaji
P.O.Box 3004,**

**Tel.: 255-23-2604617
Fax: 255-23-2604562 E-Mail:
dasp@suanet.ac.tz; www.suanet.ac.tz**

SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE (SUA)



UTUNZAJI BORA WA SUNGURA



**Idara ya Sayansi ya Wanyama na Uzalishaji
Chuo kikuu cha Sokoine Cha Kilimo
Morogoro**

FAIDIKA NA SUNGURA

- Hutoa nyama nyingi kwa haraka
- Nyama nyeupe isiyo na mafuta mengi
- Huzaa watoto wengi kwa mwaka
- Umbile lake ni dogo na rahisi kumfuga
- Ulishaji wake ni wagharama ndogo
- Nyumba ni rahisi kujenga na ghalama ndogo
- Mbolea bora ya mashamba kutokana na kinyesi
- Ngozi hutoa vifaa mbalimbali

EPUKA GHARAMA KUBWA ZA UFUGAJI


- Chagua sungura bora
- Jenga nyumba bora
- Zalisha mara kwa mara
- Lisha chakula bora

CHAGUA SUNGURA BORA

Aina zifuatazo hupatikana hapa Idara ya Sayansi ya wanyama na uzalishaji SUA:-


New Zealand White

Ni wakubwa (uzito kilo 3–5) mweupe na mwenyemacho mekundu. Huzaa watoto 8–10 kwa mzao mmjoja. Ni mweupe mwili mzima ana nyama nyingi



California

Ni mweupe na mabaka meusi puani, masikioni na miguuni, ana nyama nyingi.



Chinchilla

Ana rangi ya kahawia na ukanda wa rangi nyeusi mgongoni. Ana nyama nyingi huzaa watoto wengi



DUTCH

Wana rangi tofauti mfano kahawia, nyeusi, kijani, nk ni shupavu na wana miili midogo

Mchanganyiko

Hupatikana baada ya kuchanganya dam

JENGA NYUMBA BORA

Unapojenga nyumba, hakikisha ina mahitaji yote muhumu, hewa ya kutosha, paa la kuzuia jua na mvua na kingo kuta za kuwakinga sungura na upepo na baridi, pamoja na wanyama waharibifu. Tumia waya meshi maeneo ya joto na mbao kwenye maeneo ya baridi



Kumbuka kuwa watoto wa sungura wanazaliwa bila manyoya na wanakuwa hawaoni. Boksi au kisanduku cha kuzalia ni muhimu sana

